

Elewa mnyororo wa thamani

Watu wengi wanahusika katika kuchukua bidhaa za kilimo toka kwa mzalishaji mpaka kwa mlaji/mtumiaji
Watu wote hawa ni sehemu ya mnyororo wa soko unaowaunganisha wakulima mpaka kwa walaji/watumiaji

Fikiria kuhusu:


- Wadau wapi wanahusika katika mnyororo wa soko lako?
- Kila mdau ana kazi ipi?
- Faida ipi anayoipata kila mdau katika mnyororo wa thamani?
- Je, unajua bei tofauti katika hatua mbalimbali?
- Je, unaweza kuwaacha baadhi ya wadau wa mnyororo wa thamani?
- Jinsi gani tunavyoweza kuwaleta pamoja wadau wa mnyororo?

Kila mdau wa mnyororo wa thamani:

- Ana kazi na maslahi
- Hutaka faida kwa thamani anayoiongeza kwenye mnyororo
- Lazima awe na mahusiano imara na wadau wengine
- Lazima awe na utayari kugawana faida na hasara
- Lazima ashirikiane na kujenga uaminifu katika mnyororo

Kwanini ni muhimu kwa wakulima kujua mnyororo wa soko:

- Kuchagua mnyororo bora zaidi wa thamani, baadhi ya mnyororo ina faida zaidi kwa wakulima kuliko mingine
- Kufahamu fursa kwa wakulima (kupata faida zaidi kwa kuruka baadhi ya hatua)
- Kufahamu hatari na utalamu wa kila mdau katika mnyororo



Watoaji huduma
wuzaji wa pembejeo
Huduma za kibenki
Wagani, washauri, watafiti,...

Ongeza kipato kwa kujipanga kuchukua baadhi ya majukumu na kufupisha mnyororo wa thamani!